



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA

UFAPANUZI KUHUSU DAWA NA VIFAA TIBA VINAVYODAIWA KUONDOLEWA KWENYE KITITA CHA MAFAO CHA NHIF CHA 2023


Dar es Salaam, Machi 11, 2024

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unapenda kutoa ufapanuzi kuhusu taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoonesha orodha ya dawa 176 na vifaa tiba zinazodaiwa kuondolewa kwenye kitita cha mafao cha NHIF cha mwaka 2023. Mfuko unatoa ufapanuzi kama ifuatavyo:-

1. Maboresho ya Kitita cha Mafao cha NHIF cha 2023 yamezingatia Mwongozo ya Tiba Nchini (STG) na Orodha ya Dawa Muhimu za Taifa (NEMLIT) ambayo mwongozo wake umepitishwa na Kamati ya Kitaifa ya Wataalam iliyofanya mapitio mwaka 2021 ya dawa zote muhimu zinazotumika nchini ambapo NHIF inapaswa kuzingatia mwongozo huo.
2. Kati ya dawa 176 zinazodaiwa kuondolewa kwenye kitita cha NHIF, jumla ya dawa 134 hazipo kwenye NEMLIT, dawa aina 29 muundo wake (formulation) haijajumuishwa katika NEMLIT, dawa aina 8 muunganiko wake (combination) haujajumuishwa kwenye NEMLIT na dawa aina 3 zipo katika kitita kilichoboreshwa cha NHIF cha 2023 ambacho kinatumika sasa.
3. Aidha, Kitita cha NHIF cha 2023 kimejumuisha mbadala wa dawa husika kulingana na mwongozo.
4. Vifaa tiba ambavyo vimeainishwa kwenye orodha inayosambaa vimejumuishwa katika Kitita cha NHIF cha 2023 na baadhi gharama zake zimejumuishwa kwenye bei ya huduma husika.

Kwa taarifa hii, Mfuko unapenda kuwatoa hofu wanachama wake kwa kuwa kitita kimezingatia huduma zote muhimu hivyo unawataka waendeleo kupata huduma na endapo kutatokea changamoto yoyote wasisite kuwasiliana na ofisi ya NHIF iliyo karibu au kwa kupiga simu ya huduma kwa wateja 199.

Imetolewa na;


Anjela Mziray

MENEJA UHUSIANO